# JARIBIO LA MTIHANI WA BUNGOMA

## DARASA LA NANE MUHULA WA PILI - 2019

## KISWAHILI: LUGHA

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO** *MUDA: SAA 1 DAK. 40*

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika hii ya maswali

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**

   **JINA LAKO**

   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotegea mwanzo wa karatatsi ya majibu
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D, Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari kwenye kisanduku chenye herufi uliochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano**

    25. Mbili kipeo cha nne ni sawa na

    A. Nane B. Kumi na sita C. Sita D. Thelathini na mbili

    Jibu sahihi ni **B**

    **11.** [A] [B] [C] [D] **15.** [A] [B] [C] [D] **17.** [A] [B] [C] [D] **25.** [A] ~~[B]~~ [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 25, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari

11. Chora kistari chako vizuri, kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne uliovyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 6 zilizopigwa chapa**

**FUNGUA UKURASA**

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nufasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Msingi___1_____adabu___2_____kwa mtoto ni___3_______ ___4_______humwongoza na ___5_____ mtoto kuwa mwema. Wema ___6_____wa mtoto___7_____utakaomfanya___8_____vizuri hatimaye kuwa mtu ___9_____wa kusifika maishani. Malezi mema ni sawa na upalilizi wa ___10_____ shambani. Tabia mbaya na utovu wa nidhamu ___11_____mwanadamu ni sawa hasa na magugu au kwekwe katika konde ___12_____ mimea. Mtoto alelewe vyema ili aelewe maadili. Waovu tuwaonao walipata malezi ___13_____ . Naam mtoto umleavyo ndivyo ___14_____ . Adabu hupaliliwa! Usipopalilia shamba miche na mimea___15_____vizuri kamwe!

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | wa | ya | la | za |
| 2. | mwema | njema | vyema | mzuri |
| 3. | mlezi | malezi | ulezi | kuka |
| 4. | mwema | mzuri | mema | mabaya |
| 5. | kumwelekeza | kumtekeleza | kuwaelekeza | kumteleza |
| 6. | hii | huu | huo | hizi |
| 7. | ndiyo | ndilo | ndio | ndicho |
| 8. | akuwe | akue | awe | hakue |
| 9. | mbora | wabora | bora | boya |
| 10. | michi | miche | machi | gugu |
| 11. | kwa | katika | kuwa | kwenye |
| 12. | cha | za | ya | la |
| 13. | mazuri | mzuri | wazuri | mabaya |
| 14. | akuayo | akuaye | akuavyo | huwa |
| 15. | hukuwa | haikui | haikuwi | hukwa |

**Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililosahili**

16. Ni sentensi ipi imezingatia matumizi ya Kwa kama Kihusishi?
   A. Wake kwa waume wamesusia mgomo
   B. Mwanafunzi ameenda kwa mwalimu
   C. Watu kumi kwa ishirini wanaugua ukimwi
   D. Ataenda Nairobi kwa gari
17. Ni maelezo yapi mufti kulingana na msamiati wa utaifa
   A. Mlowezi - Mtu aliyehamia nchi nyingine
   B. Bepari - Adui wa haki na nchi yake
   C. Mzalendo - Asiyependa nchi kwa dhati
   D. Mwenyeji - Mgeni wa sehemu fulani
18. Ni neno lipi kati ya haya si kitawe ?
   A. Mbuzi B. Fema
   C. Matwana D. Kama
19. Wali, ugali. nyama na kande ni vyakula. Je shakwe, mumbi, keremkerem na koho kwa jina moja ni
   A. maua B. magari
   C. mavazi D. nyuni
20. Ni sentensi ipi imetumia Kirejeshi 'O' kwa usahihi?
   A. Mtu ambaye aliyekuja ni mtundu
   B. Kiti ambacho kiliyopotea kimepatikana
   C. Gari ambalo limenunuliwa ni ghali
   D. nyuzi zilizotumiwa hazipendezi
21. Andika tarakimu kwa maneno: 20,002
   A. Ishirini na mbili elfu
   B. Ishirini elfu na mbili
   C. Elfu mbili na mbili
   D.Mia mbili na mbili
22. Chagua aina ya pambo ambalo huvali wa
   A. kidani B. kipini
   C. nembo D. kibanio
23 Wingi wa sentensi :-
   Ufa uliozibiwa zilikuwa pana
   A. Nyufa tuliozikuwa pana
   B. Nyufa zilizozibiwa zilikuwa pana
   C. Maufu yaliyozibiwa yalikuwa mapana
   D. Nyufa ziliyozibiwa zilikuwa pana
24. Ala ya muziki inayofanana na gitaa lakini yenye tumbo huitwa
   A. zumari B. kayamba
   C. dumbaki D. udi
25. Kitendawili " Nala vyote vinono lakini sikui wale kunenepa"
   A. chungu cha kupikia
   B. nyweleni kichwani
   C. magurudumu
   D. mafiga na chungu
26. Chagua jibu linaloonyesha sehemu ya mshororo katika mashairi
   A. kibwagizo, malenga
   B. mloto, mleo
   C. tasidisa, utenzi
   D. kipokeo kituo
27. Chagua sentensi iliyo kisarufi
   A. Ameenda katika nyumbani kwao
   B. Mwanafunzi ametumwa kwa duka
   C. Abiria ameingia ndani ya garini
   D. Wazee wamekaa katika baraza
28. Yapi si maelezo sahihi ya istilahi za lugha
   A. Kivumishi : Neno linalotoa maelezo zaidi kuhusu nomino.
   B. Kiambishi : Kipande cha neno huwa ni silabi
   C. Kihusishi : Neno linaloonyesha uhusiano
   D. Kiingizi : Neno ambalo halitumiwi kuonyesha hisia
29 Endapo aliyehukumiwa walidhishwi na hukumu iliyotolewa anaweza kukata
   A. wakili
   B. dhamana
   C. rufani
   D. uamuzi
30 Mtoto mzembe ameenda masia. Maana yake ni
   A. Amekuwamwisho katika mtihani
   B. Ameishi miaka mingi
   C. Ameona wivu kutokana na jambo zuri
   D. Ameenda kwa miguu

***Soma kifungu kifuatacho kisliu ujibu muswali 31- 40***

Utalii ndio njia moja wapo ya kujipati fedha za kigeni nchini Kenya. Kila mwaka, mamilioni ya wageni hujanchini kutoka Ugereza, Marekani. Ujerumani na kwingineko. Mbali na kujionea jinsi maisha yalivyo katika miji na mashamba, watalii hupata nafasi tele ya kutembelea sehemu za nchi kuliko na wanvama pori kama simba ,ndovu, chui, kifaru, mamba na kiboko.

Sehemu hizi za mbuga za wanyama zimehifadiwa na serikali na wanvama waliomo hulindwa na sheria za nchi. Sababu ni kvvamba wanyama wengi wanaopatikana katika mbuga hizi huwindwa sana kwa ngozi au pembe, vipusa na kwato zao. Pembe za ndovu, ngozi ya simba na chui meno ya mamba na hata ngozi yake, ni vitu vya thamani kubwa katika nchi nyingi za ulimwengu.

Wawindaji haramu huwafuata wanyama hawa mchana na usiku ndipo wapate kuwaua na kuuza ngozi na pembe. Ni hasara kubwa sana nchi kama yetu ikipoteza wanyama hawa. Kwanza. watalii hutembelea nchi hii. Inatoa ikumbukwe kwamba watalii hutembelea nchi yetu kwa sababu kwao hawana mbuga za wanyama kama huku kwetu.

Mbuga za wanyama kama za Tsavo, Amboseli, Masai Mara, Nairobi. Meru na Mlima Keny a zinajulikana ulimwenguni kote kama mahali pa kutazama wanyama hawa. Wageni wanapokuja hukaa katika hoteli zilizojengwa katika sehemu hii ya nchi yetu, chakula malazi na hata kusafiri kwao ni njia zinazoleta faida kubwa kwa nchi.

Isitoshe, kama wanyama hawa wangewindwa wakaisha. wajukuu wetu wangepata hasara kubwa. Wasingepata nafasi ya kuona mnyama kama simba au ndovu akiwa hai katika mazingira yake. Ingekuwa ni kutegemea picha ili mtoto afahamu mnyama anayezungumziwa. Hili lingekuwa kosa kubwa kwa kizazi cha leo. Serikali imetfanya jitihada kubwa tangu mwaka 1976 kuhakikisha kwamba wawindaji haramu hawapati nafasi kwa kumaliza biashara yoyote inayohusiana na pembe, vipusa au ngozi za wanyama.

31. Kulingana na kifungu katika aya ya kvvanza
    A. Utalii ndio njia pekee ya kujipatia fedha za kigeni nchini.
    B. Watalii huja Kenya kutoka Uingereza. Marekani, Ujerumani pekee.
    C. Watali huja kutembea sehemu za nchi kuona warryama pekee.
    D. Tembo ni mojawapo ya wanyama wanaopatikana nchini.

32. Neno **Vipusa** limetumiwa katika aya ya pili. Maana yake kulingana na taarifa ni.
    A. Pembe ndogo ya kifaru
    B. Msichana au mvvanamke mrembo
    C. Aina ya mnyama mkali
    D. Pembe ndogo za vifaru

33. Jinsi jingine la wawindaji haramu ni
    A. Majangili B. Majanguo
    C. Janabi D. Jaramandia

34. Ni hasara gani nchi itapata kutokana na wanyama kuuawa?
    A. Pembe na ngozi kunzwa
    B. Watalii kutotembelea taifa letu
    C. Wananchi kuandamana barabarani
    D. Kukosa mbuga za wanyama nchini

35. Kwa nini wanyama hulindwa na sheria za nchi?
    A. Ili wasitoroke mbugani
    B. Kwa sababu wengi ni hatari
    C. Ili wanyama hawa wasisakwe
    D. Kuhifadhi pembe na ngozi za wanyama

36. Tunaposema vitu vya thamani tuna maanisha
    A. Gharama au ubora wa kitu kutokana na hali
    B. Tia gharama au bei ya kitu
    C. Wekea ahadi mtu kama atatimiza jambo Fulani
    D. Mwezi wa mwisho wa kasi

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

37. Mbali na kifaru kuwa mnyama pia ni
A. Gari lachuma la kivita
B. Kitu kinachotumiwa kufungia vazi
C. Malipo ya awali yanayotolewa kwa mganga
D. Nyumba ambayo mtoto wa nondo hukaa

38. Kati ya wanyama waliotajwa katika kifungu wapi wanaishi majini
A. Ndovu, chui. mamba
B. Simba, mamba, kiboko
C. Samaki, mamba. kiboko
D. Ngwena, kiboko

39. Ni hasara gani wajukuu watapata iwapo wanyama wangewindwa wakaisha?
A. Nchi itapoteza pesa za kigeni
B. Watakosa fursa ya kuwaona wanyama
C. Ndovu na simba hawatakuwa katika mazingira yao
D. Serikali itafanya jitihada ya kuzuia wanyama kuwindwa

40. Kichwa mwafaka cha habari hii ni kipi
A. Utalii
B. Wanyama pori
C. Wawindaji haramu
D. Fedha za kigeni

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.**

"Hamjambo wananchi.

Nimefurahi sana kuona mlivyojitahidi kufika kwenye mkutano huu. waume kwa wake. Nimewaita ili kuwahutubia juu ya uhalifu ambao umeongezekana sana.

Wiki iliyopita Mzee Makanya alivamiwa na wakora akapigwa nusura afe, akanyang'anywa kila kitu. Juzi majambazi thelathini walienda kuvunja duka la Mwinyi Hatibu wakamwua mlinzi wa duka hilo na kuiba mali yake vote. Wasichana wetu hawana uhuru wa kutembea njiani, huwa wananajisiwa na kubakwa. Kuna mambó mengi sana ya uhalifu yanayotendeka. Sasa nimewaita ili niwaeleze vile tunayoweza kukiumbana na matatizo haya. Tukishirikiana sote tutaweza kuwashinda wahalifu kwa sababu ushirika ni nguvu na kidole kimoja hakiwezi kuvunja chawa.

Kila mtu yamfaa awe macho. Ukisikia makelele kwa mwenzako, sote wanakijiji tutoke nje na silaha tuwasake wahalifu. Mtoke kwa ujasiri lakini pia kwa hadhari ili tusijeruhiwe na majambazi. Mkimwona mhalifu mnyemfahamu, pelekeni ripoti zenu kwa chini ili mienendo ya mtu huyo ichunguzwe.

Tunataka mji wetu uwe wa salama na amani ili kila mtu aweze kutembea bila wasiwasi ikiwa ni mchana au usiku. Uhalifii mwingine ambao umetufika ni kuhusu vijana wetu. Inasikitisha kuwaona watoto wetu wakiwa na vichwa vikubwa na kuvuta sigara, bangi na wanatumia vileo vingine vikali na pombe. Wakiwa katika hali ya ulevi, hawajali maisha yao au ya wenzao.

Watoto wetu wa kike wanapata mimba ovyo mara nyingine wakiwa wachanga sana. Magonjwa ya zinaa yameongezeka kupindukia. Siku hizi kuna ugonjwa mpya wa zinaa. Ukimwi, ambaó ni ukosefu wa kinga mwilini. Wiki iliyopita katika hospitali yetu ya mtaa kijana wetu wa kijiji ni mpendaye amefariki kwa ugonjwa huo. Masikitiko makuu!

Tatizo hili si la mzazi mmoja, ni letu sote. Kwa kutatua matatizo haya tumekomesha kuuza sigara na pombe kwenye maduka yetu. Wauguzi wameongezwa ili kumpima kila mtu awe ni baba, mama au mtoto kuhakikisha kuwa hawana magonjwa mabaya. Wale walio na magonjwa mabaya watahamishwa kuishi peke yao mpaka wapone. Nawaomba watu wote tuungane mikono ili tuondoe uhaliru katika kata yetu. Asanteni kwakunisikiliza."

41. Ni kweli kusema kuwa

A. Mzee Makanyaga alipigwa akafa

B. Wezi themanini walivamia duka la mwinyi Hâtibu

C. Utengano unawezesha wahalifu kushindwa

D. Mabanati wanahofu ya kutembea njiani

42. Kila mtu anastahili kuwa macho kwa sababu

A. ili aweze kusikia makelele usiku

B. ili aweze kusaka majambazi bila tahadhari

C. ili kushirikiana kusaka wahalifu lakini kwa tahadhari

D. wezi huvamia kijiji kila siku

43. Ipi katika magonjwa hata si ya zinaa

A. ukimwi

B. kaswende

C. kisonono

D. pepopunda

44. Mji ukiwa na usalama na amani

A. Watu wataishi kwa umoja na upendo

B. Watu watatembea usiku kucha pekee

C. Watu watatembea mchana bila uoga

D. Watu watatembea siku nzima bila wasiwasi

45. Madhara yapatikanayo kwa binadamu kulingana na kifunguni?

A. Kutumia dawa za kulevya

B. Watoto kuwa na vichwa vikubwa

C. Kila mtu kuhakikisha hana magonjwa mabaya

D. Kushiriki katika kuwasaka wahalifu

46. Tunaposema watoto wetu watakuwa vichwa vikubwa tuna maanisha

A. Vichwa vyao vitakuwa vizito na vikubwa

B. Vijana wetu watakuwa watukufu

C. Vijana wetu watakuwa wajeuri

D. Vijana wetu hawatakuwa watundu

47. Hotuba hii ilitolewa na nani kwa hadhira

A. Rais

B. Chifu

C. Polisi

D. Mhalifu

48. Kijana aliyependwa sana alikata kamba kutokana na ndwele upi?

A. Uhalifu

B. Ukimwi

C. Malaria

D. Zinaa

49. Njia kuu ya kukumbana na matatizo yanayokumba mji ni

A. Kutoshirikiana

B. Kutokuwa na umoja

C. Kuwa na umoja

D. Kusaka wahalifu

50. Kichwa kifaacho habari hii ni

A. Uhalifu

B. Hotuba

C. Zinaa

D. Vijana